# TARGETER WINGS

## JUNIOR SCHOOL ASSESSMENT

## GREDI YA NANE - 2024

Wings 004

## KISWAHILI

**Muda: Saa 1 dakika 20**

**Jina** ______________________________

**Shule** ______________________________

**Nambari ya Usajili:** ________________ **Tarehe** ________________

**Maagizo**

*(a) Andika jina lako, la shule, nambari ya usajili na tarehe kwenye vihasho uliopewa.*

*(b) Jibu maswali yote kwenye karatasi hili.*

| MTAHINI PEKEE | | | |
|---|---|---|---|
| **Swali** | **Upeo wa alama** | **Alama ya mwanafunzi** | **Kiwango cha utendaji** |
| 1-29 | Alama 50 | | |
| **Jumla** | **50** | | |

**I. UFAHAMU WA KUSOMA**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 hadi 4:***

Mbogo na Buibui walikuwa wakiishi katika msitu mmoja. Siku moja, msitu huo ulishika moto. Wanyama wote walishikwa na wasiwasi mkubwa. Wakaanza kutoroka ili wajiokoe. Mbogo alipokuwa akikimbia, alikutana na buibui aliyekuwa amejawa na hofu tele kutokana na ongezeko la moto. Buibui alimwambia Mbogo, "Nakuomba bwana Mbogo kwa hisani yako unichukue juu ya pembe zako nisiteketee, nami nitakusaidia siku za usoni." kumbuka, "Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki".

Mbogo hakuamini kauli ya Buibui. Alidhani kuwa Buibui alimtania. Kwa kejeli alimjibu,"haya basi, kidudu kama wewe utanifaa vipi? Wewe unajidai tu." Baada ya kuwaza na kuwazua, Mbogo alimhurumia na kumbeba. Wote wakasalimika. Wakaendelea kuishi pamoja kama ndugu wa toka nitoke.

Siku moja marafiki hawa walipokuwa wakitembea tembea msituni, walisikia wawindaji wakimsaka Mbogo. Hofu ikamwingia Mbogo akashindwa la kufanya. Buibui alipomwona rafiki yake akihangaika, akamwambia. "Usifadhaike moyoni, kwendako hisani hurudi hisani hakurudi nuksani. Ni wakati wangu wa kulipa fadhili kwa wema ulionitendea. Wawindaji walipokaribia, Buibui alianza kuzificha nyayo za Mbogo kwa kuzizungusha utando. Wawindaji walipofika pale palipokuwa na utando, walishindwa iwapo nyayo hizo zilikuwa za wakati huo. Wakageuka na kuelekea kwingine. Mbogo alimshukuru na kugundua kuwa kitendo chake cha awali cha kumdharau na kumkejeli Buibui hakikuwa na mashiko.

1. Mbogo na buibui walikabiliwa na hatari gani?

   ______________________________

2. Mbogo aliepukaje wawindaji waliokuwa wakimsaka?

   ______________________________

3. Je, mbali na moto inayowakabili wanyama wa mwituni, andika hatari nyingine inayowakabili wanyama

   ______________________________

4. Jina jingine la mbogo ni lipi?

   ______________________________

**II.** ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 5 hadi 8.***

Usalama nyumbani ni muhimu maishani. Jambo lililo hatari zaidi ni uhalifu unaofanyika nyumbani. Uhalifu ni hali ya uvunjaji sheria za nchi au jamii. Anayevunja sheria ni mhalifu. Mhalifu hapendwi na wengi maadam anaaminika kuwa ni mtu wa kuvuruga raha na heshima ya wenzake. Mtu sampuli hii hukosa hata mtu wa kumshauri kwa kuwa wengi huogopa kushirikiana naye.

Mwizi ni mhalifu anayevunja sheria. Atafika nyumbani kwako kwa kisingizio cha kukujulia hali kumbe amekuja kuchunguza jinsi hali ya kwako ilivyo. Baadaye akishapata ***ramani*** ya nyumba yako hutokomea kwenda kuandaa kikosi na kurejea baadaye kutekeleza uhalifu kwa kudanganyika na ubinadamu bandia aliokuonyesha, utashtukia ukikabiliwa na mikasa ya wizi wa mabavu, na huenda hata ukapoteza uhai.

Watu wanaowaajiri watoto nyumbani na kuwafanyisha kazi ngumu huvunja sheria na kuhatarisha usalama wao. Huo ni ukiukaji wa haki za watoto. Mkono wa sheria utakapowaandama watalazimika kujuta. Hata hivyo watakuwa wamechelewa; majuto ni mjukuu huja kinyume.

Wazazi wasiowapeleka watoto wao shuleni waelewe kuwa usalama wao nyumbani hautabiriki. Watamalizia kuwa wahalifu. Vitina vya nyumbani huhatarisha usalama. Uwepo wa ua hauzuii uhalifu kutendeka nyumbani. Ni muhimu pia kuhakikisha kuwa makazi yetu yanaepushwa na mambo yanayoweza kusababisha ajali kama vile mioto, kuteleza na kuanguka au milipuko.

**5.** Kulingana na kifungu, ni jambo gani linalohatarisha usalama nyumbani?

____________________________________________

**6.** Ni kauli ipi kutokana na taarifa hii isiyo ya kweli? ____________________

A. Ajira kwa watoto ni kinyume cha sheria.
B. Nyumba inayozungukwa na ua haina usalama wowote.
C. Mwizi ni mhalifu kwa kuwa huiba.
D. Baadhi ya wageni wanaokuja kukujulia hali wanaweza kuwa wahalifu.

**7.** Kifungu kimebainisha kuwa uhalifu ni hatari na haupendwi katika jamii. Je, unadhani ni kwa nini wahalifu hutengwa katika jamii?

____________________________________________

**8.** Neno, **'ramani'** limetumika katika kifungu. Ramani ni ____________________

A. eneo au mahali kitu kilipo  B. ufahamu wa sehemu fulani
C. njia inayoelekea sehemu fulani  D. picha au taswira ya mahali.

**III. UFUPISHO**

***Soma kifungu hiki kisha ujibu swali la 9 hadi 12.***

Mawasiliano ni neno pana zaidi. Mawasiliano ni taaluma inayowawezesha watu kupashana habari, kupokezana ujumbe, kupokezana mizigo na hata kujuliana hali. Kuwasiliana kupo kwa mikondo tofauti na mipana kidogo kuliko tunavyodhani.

Barabara zikiwa mbaya, utawasikia watu wakisema kuwa mawasiliano katika sehemu fulani ni mabovu. Njia zikiwa mbaya, sekta zote huathirika kuanzia elimu hata biashara. Hakika, hakuna msiba u siokuwa na mwenzake. ***Vyombo vya habari kama vile redio, runinga, magazeti, majarida na mitandao ya kijamii ni vipengele muhimu vya mawasiliano***. Habari zilizomo na yanayojiri kutoka sehemu tofauti tofauti za ulimwengu hufahamika kwa upesi na wakati ufaao. Je, kusingekuwa na vyombo hivi vya mawasiliano, habari za ulimwenguni zingejulikana namna gani?

Barua zilizotumwa kwa njia ya posta zimekuwa muhimu lakini mabadiliko ya kiteknolojia hasa intaneti yameathiri njia hii ya mawasiliano. Mtu anaweza kutuma barua katika pembe yoyote ya dunia na kupokea majibu papo hapo kwa kutumia barua pepe.

Barua hizi aghalabu hutumwa kupitia tarakilishi. Mbinu hii imebadilisha dunia na kuifanya kuwa kama kijiji kidogo. Ulimwengu mzima unaunganishwa kupitia utandawazi hivi kwamba tukio lolote kwenye sehemu moja hujulikana upesi kote ulimwenguni. Aidha rununu ni njia nyingine ya mawasiliano ambayo inapendwa na watu wengi. Hii ni njia iliyo rahisi kutumiwa na watu wengi.

**9.** Ni kichwa gani kinachofaa kifungu hiki?

____________________________________________

**10.** Eleza maana ya mawasiliano kwa maneno yasiyozidi 12

____________________________________________

**11.** Kauli, ***Vyombo vya habari kama vile redio, runinga, magazeti, majarida na mitandao ya kijamii ni vipengele muhimu vya mawasiliano***. Imetumika katika kifungu, fupisha kauli hii kwa maneno yasiyozidi 8

____________________________________________



CamScanner

12. Andika habari kuu inayojitokeza katika aya ya tatu kwa sentensi moja.

_______________________________________________

## IV. TAMTHILIA

13. ***Sehemu hii ina dondoo lililotolewa kutoka kwenye moja kati ya tamthilia zilizoidhinishwa kwa wanafunzi wa Gredi ya 8. Jibu maswali yote ya dondoo hili.***

**Mabula** : Sasa swali gani hilo?

**Mishi** : *(Kwa msisitizo)* La iwapo mimi ni nani kwako maana ninaona unanifanya mimi prefect wa watoto wanaocheza. Sijui kama ni class prefect, games prefect au music prefect!

**Mabula** : Sasa imekuwa ni hayo?

**Mishi** : Ndiyo haya uliyaanza wewe. Ningekuwa mke kwa maana ya mke usingeniweka kundi sawa na watoto.

**Mabula** : *(Anacheka kicheko kirefu)* Mishi, ninashindwa kuelewa kwa nini mambo madogo yanakuchenga.
Usipowapa watoto mwongozo atawapa nani?
Hebu niambie.

**Mishi** : Mwongozo katika michezo ya watoto?

**Mabula** : Mishi, usidharau nguvu za nyimbo. Wanasema mwanzo wa ngoma ni lele.

**Mishi** : Basi kama ni lele, nimeicheza sana hiyo lele!

**Mabula** : *(Ameukinai mjadala)* Ushindani wa namna hii hauwezi kutufaa kitu. Angalia muda wote huu umekuwa ni mvutano usiokuwa na msingi. Tumeharibu muda mwingi kubishana. Hivi ubishi utatufaa nini?

a) Katika mazungumzo haya, Mishi ni nani kwa Mabula?(alama 1)

_______________________________________________

b) Chanzo cha mzozo kati ya Mishi na Mabula ni: (alama 1)

_______________________________________________

c) Maudhui ni masuala ambayo yanazungumziwa katika kazi ya fasihi. Eleza masuala mawili yanayojitokeza katika dondoo hili (Alama 2)
i) _______________________________________________
ii) _______________________________________________

d) Eleza mbinu nne za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili (alama 4)
i) _______________________________________________
ii) _______________________________________________
iii) _______________________________________________
iv) _______________________________________________

e) Tambua sifa mbili za Mishi kulingana na dondoo hili. (alama 2)
i) _______________________________________________
ii) _______________________________________________

## V. SARUFI

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 14 hadi 18. Umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Maadili ya kijamii huleta ___14___. Watoto___15___ na maadili huibuka kuwa watu wazima ___16___ maisha. Hatuwezi kungoja hadi mtoto afikie umri wa makamo ndipo aanze ___17___ maadili. Kumbuka waswahili husema, '___18___'.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 14. | A. utengano | B. utangamano | C. misukosuko | D. utengamano |
| 15. | A. inayolelewa | B. wanayolewa | C. wanaolewa | D. wanaolelewa |
| 16. | A. wanayoyathamini | B. wanaodhamini | C. wanaoyatamani | D. wanayoyadhamini |
| 17. | A. kufunza | B. kufuzu | C. kujifunza | D. kusomea |

18. A. Ukiona vyaelea jua vimeundwa
B. Jifya moja haliinjiki chungu
C. Kichango ni kuchangizana
D. Samaki mkunje angali mbichi



CamScanner

19. **Chagua nomino ya wingi iliyo kwenye kadi hii**

| | |
|---|---|
| **Halaiki** | **Miti** |
| **Wema** | **Unga** |


20. Sentensi, **"Maskini!** Kwani unaugua kipindupindu?" Imetumia alama ya hisi. Je ni aina gani ya hisia inayojitokeza katika sentensi hii?

21. **Pigia mstari kiwakilishi kionyeshi katika sentensi:**
Mle mna dawati lile lililotengenezwa na seremala

22. Maneno ghali na gali yametumia sauti /g/ na /gh/. Tunga sentensi ukitumia maneno ghani na gani ili kuzitofautisha sauti hizi.

23. Sentensi, "Kitanda hakijatandikwa" ipo katika hali timilifu. Iandike upya sentensi hiyo katika hali ya mazoea.

24. Chagua kivumishi ambacho hakipaswi kuwa katika kapu hili.




25. Andika sentensi: "Mazulia hayo yao yalifumwa na washonaji wale" kwa umoja

26. Maneno yafuatayo yanafuatana vipi katika kamusi?
**i) Mshtakiwa  ii) Umma  iii) Uma  iv) Umio  v) Mashtaka**

27. Ikiwa juzi ilikuwa Alhamisi, mtondogoo itakuwa siku gani?

28. Andika kauli ifuatayo katika usemi taarifa.
"Soko litasafishwa lini?", Charo akauliza.

**VI. FASIHI (Alama 20)**

29. a) Novela hutofautianaje na tamthilia? (alama 2)
i)
ii)

b) Eleza namna bembelezi inavyowasilishwa ukirejelea mambo yafuatayo (alama 3)
i) Sauti
ii) Urudiaji
iii) Miondoko ya mwili

c) Andika sifa mbili za mighani katika jamii yoyote (alama 2)
i)
ii)

d) Eleza tofauti kati ya mighani na visasili. (alama 2)
i)
ii)

e) Wahusika wana jukumu gani katika kazi ya fasihi? (alama 1)



CamScanner

# TARGETER WINGS

## JUNIOR SCHOOL ASSESSMENT

# GREDI YA NANE - 2024

Wings 004

## SEHEMU B:

## KISWAHILI : INSHA

***MUDA: Dakika 40***

| | |
|---|---|
| **Jina** ______________________________ | |
| **Shule** ______________________________ | |
| **Nambari ya Usajili:** ________________ | **Tarehe** ________________ |

**SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI**

1. Kwenye nafasi zilizoachwa hapo juu **andika jina lako na jina la shule yako.**

2. Sasa fungua karatasi hii, soma kichwa cha insha kwa makini na uandike insha yako kwenye nafasi uliyoachiwa.

**Kijitabu hiki kina kurasa 4 zilizopigwa chapa.**

*© Hutungwa na kuchapishwa na Targeter Educational Publishers Ltd. Email:info@targeterpublishers.co.ke*

**FUNGUA KURASA**

CamScanner

***Andika insha itakayomalizia kwa maneno haya.***

................ *ziara hiyo kwa mjomba ilikuwa ya kufana.*



CamScanner